**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS TAMISEMI**

SHULE YA SEKONDARI MUYOVOZI,
S.L.P 463,
**KASULU**

28/03/2022.

**Kumb.Na.MYVZSS/S4684/VOL.9/1**
**Mawasiliano:**
**Mkuu wa shule: 0757932910/0622032538/0786115939**
**M/Mkuu wa shule: 0629118414**
**Mhasibu wa shule: 0620392864/0764200814**
**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi................**

**S.L.P..............................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUYOVOZI HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU MKOA WA KIGOMA MWAKA 2022/2023**

## 1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya ………….

Shule ipo Kilometa 44 Kutoka Kasulu Mjini kuelekea barabara kuu iendayo Kibondo, Mwanza, Arusha, Moshi, Singida, Dar Es Salaam n.k. Washuke kituo cha **Mgombe** sokoni kama unatokea Kasulu Mjini au unashukia kituo cha njia panda ya kwenda Kambi ya jeshi la kujenga Taifa **(JKT) Mtabila** katika kijiji cha Mugombe. Ambapo nauli kutoka Kasulu Mjini hadi Mugombe sokoni ni shilingi elfu tatu (3,000/=) kwa magari madogo ya abiria na shilingi elfu tano (5,000/=) kwa pikipiki kutoka Mugombe hadi shuleni. Pia unaweza kukodi usafiri au gari dogo kutokea Kasulu Mjini kwa shilingi elfu thelathini (30,000/=) inategemea na makubaliano yenu.

Muhula wa masomo utaanza mwezi ………………, hivyo fika mapema iwezekanavyo ili shule ikifunguliwa tarehe …………….2022 masomo yataanza mara moja**.**

## 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:

### 2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule kwa; **WAVULANA** ni suruali nyeusi 2 au zaidi na bluu mpauko (light bluu) 2 au zaidi zenye marinda mawili na upana chini uwe wa inchi kumi na saba (17’) na mifuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma (**Modo na zisizo na marinda hazirihusiwi)** mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi, mashati mawili au zaidi meupe yenye mikono mirefu yasiyo na urembo au maandishi yoyote na tai mbili nyeusi na bluu mpauko(light bluu) mbili zinazofanana na kitambaa cha suruali na usinunue spesho. **WASICHANA** ni sketi nyeusi 2 au zaidi na bluu mpauko (light bluu) 2 au zaidi ndefu zinazofikia jicho la mguu zenye rinda boksi mbele na nyuma na sio V ya mbele, mashati meupe 2 au zaidi yenye mikono mirefu yasiyo na maandishi au urembo wowote, tai 2 za bluu mpauko na tai 2 nyeusi. Kwa

**wasichana wa kiislamu** shona nusu kanzu nyeupe 2 au zaidi, nyekundu 2 au zaidi na juba nyekundu 2 au zaidi na nyeupe 2 au zaidi zinazofunika kitovu zisizo na maandishi au urembo wowote.

b) Viatu vya kufunga na kamba jozi mbili (2) au zaidi vyenye visigino vifupi
c) Nguo za kushindia:
    1. T.shirt nyeupe yenye rangi ya bluu kwenye kola na mikononi na gauni ndefu zinazofikia jicho la mguu zenye rinda boksi mbele na nyuma rangi damu ya mzee ya kitambaa kizito kwa ajili ya shughuli za nje ya darasa, soksi nyeupe jozi tatu au zaidi zisizo na urembo au maandishi yoyote kwa wasichana na nyeusi jozi 3 au zaidi kwa wavulana zisizo na urembo au maandishi yoyote.Pia wavulana waje na suruali za nje ya darasa zenye rangi damu ya mzee kitambaa kizito cha kushona na siyo spesho zenye marinda mawili na upana chini uwe wa inchi kumi na saba (17’) na mifuko miwili mbele na mfuko mmoja nyuma (**Modo na zisizo na marinda hazirihusiwi)**
d) Sweta rangi ya damu ya mzee kwa ajili ya baridi liwe zito kulingana na afya yake (hakuna makoti au masweta ya aina nyingine yoyote yatakayo ruhusiwa)
e) Mavazi ya michezo ni bukta/sketi ya bluu zisizo na marinda (solo) ambazo hazina marembo au maandishi yoyote na T.shirt nyekundu zenye kola nyeusi na ufito mweusi mikononi na kwenye mfuko zisizo na maandishi yoyote kwa wote, raba kwa wasichana na viatu vya michezo kwa wavulana.Pia wote (wasichana na wavulana) waje na tshirt(jezi) ya michezo rangi nyeusi
f) Viatu vya tope (rainboot) na mwavuli
g) Tracksuit ya rangi ya bluu kwa **wasichana** na rangi nyeusi kwa **wavulana** zisizo za kubana au marembo na **zisiwe na kofia ya kuvaa kichwani**.

**ZINGATIA:**

1. **MWANAFUNZI AWAPO SHULENI HARUHUSIWI KUVAA NGUO ZA NYUMBANI NA WALA ASIJE NAZO SIKU YA KURIPOTI BALI AJE AMEVAA SARE ZA SHULE.**
2. **PIA NI MARUFUKU KUJA SHULENI NA SIMU KWA KISINGIZIO CHA KUIKABIDHI OFISINI,UKIJA NAYO ITAVUNJWA PALEPALE NA UTARUDISHWA NYUMBANI KWA KUKIUKA MAELEKEZO HAYA .MWANAFUNZI AWAPO SHULENI ATAWASILIANA NA MZAZI/MLEZI KWA SIMU ZILIZOELEKEZWA NA MKUU WA SHULE ZILIZOANDIKWA KWENYE FOMU HII**

**2.2 Ada na Michango ya Shule**

**a)** Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000.00 kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35, 000.00 kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Namba. **51410006450** katika benki ya **NMB** jina la akaunt “**MOYOVOZI SECONDARY SCHOOL CAPITATION**” (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye payslip).

**b) Michango Inayotakiwa Kulipwa na Kila Mzazi**

i. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Shilingi 35,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
v. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule
vi. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza mwanafunzi akiugua
vii. Shilingi 20,000/= mitihani ya kujipima *mock/joint examinations*
viii. Fedha ya tahadhari shilingi 5000/=(haitarudishwa)

**Jumla ya ada na michango yote kwa mwanafunzi ni shilingi laki moja na themanini na nane (Tshs 188,000/=) kwa mwaka Angalizo: Michango hii yote ilipwe kwenye account ya shule iliyotajwa hapo juu na siyo vinginevyo.**

**c) Mahitaji Muhimu Ambayo Mwanafunzi Anapaswa Kuleta Shuleni:**

i. Ream ya karatasi mbili (2) kila mwaka,(**DOUBLE A au PREMIERS)** kwa wote aina nyingine ya Ream haitapokelewa **KAMWE**
ii. Daftari kubwa (counter books (**3 au 4 Quires** ) zinazotosheleza masomo yake, vitabu/vitini vya tahasusi yake
iii. Njoo na vitabu vya masomo yako unayosoma kwa matumizi yako binafisi na pia calculator kwa wanaosoma Mathematics na Geography
iv. Godoro 2 ½" kwa 6" aina ya **Dodoma/Banco tu** nasiyo malaika
v. Mashuka jozi mbili (rangi ya bluu bahari) kwa wote
vi. Blanketi(**asije na shuka la Maasai**), mto wa kulalia na foronya yake rangi ya bluu bahari
vii. Chandarua rangi ya bluu hasa ya mstatili
viii. Taulo, nguo za kulalia na ndala za kuogea
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
x. Ndoo mbili zenye mifuniko
xi. Kiti cha plastiki 1
xii. Taa au tochi ( inashauriwa anunue taa ya kuchaji kwa jua) kwa tahadhari au dharura
xiii. Kwanja 1 na Panga 1 lililonolewa(**kwa wasichana tu**)
xiv. Rake 1 (**kwa wavulana tu**)
xv. Jembe 1 lenye mpini na mopa 1 (ya kudekia yenye mti na raba yake) **kwa wote**
xvi. Mfagio (**hardbroom** ) **kwa wote**
xvii. Mfagio (**chelewa**) mmoja wenye mti wa kushikia **kwa wote**.

## 3.0. SHERIA ZA SHULE

Shule ya sekondari huendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu namba 25 ya mwaka 1978 iliyorekebishwa kwa nyongezaya sheria namba 10 ya mwaka 1995 .Aidha shule ya sekondari muyovozi iko makini katika kusimamia na kutekeleza miongozo yote inayotolewa na wizara uya elimu sayansi na teknolojia pamoja na miongozo ya TAMISEMI.Mwanafunzi wa muyovozi

anategemewa kuwa na maadili mema na mfano bora kwa jamiii.Hivo anatakiwa kuzingatia taratibu na kanuni zote atakazopewa shuleni.Kutokuzingatia sheria na kanuni hizo kutapelekea achukuliwe hatua mbalimbali kwamujibu wa sheria na kanuni za shule ambapo inaweza ikapelekea yeye kuadhibiwa ikiwa ni pamoja na kachishwa masomo.

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
ii. Wizi
iii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iv. Kugoma na kuhamasisha mgomo
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
vii. Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
viii. Kufuga ndevu
ix. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
x. Uvutaji wa sigara
xi. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
xii. Kujihusisha na mapenzi shuleni au kuwa na mahusiano ya kimapenzi
xiii. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xiv. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xv. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xvii. Kudharau Bendera ya Taifa
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xix. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 Usajili:**


Mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa, cheti/result slip ya kidato cha nne na akamilishe kujaza fomu zote zilizoambatanishwa na maelekezo haya. Aripoti na joining instruction na awe na picha(passport size 2)

**5.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

A. Fomu ya Kukubali Kujiunga na Shule
B. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA MUYOVOZI SEKONDARI**




**NHIGA J. MWANDU**
**MKUU WA SHULE**

FOMU B

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mzazi/Mlezi wa ............................................

..........................................................................

..........................................................................

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Muyovozi,
S. L. P. 463,
**KASULU.**

Mimi ..................................................................................... (Mwanafunzi) nimesoma kwa makini na kuyaelewa mahitaji na sheria za shule kama zilivyoandikwa.

- Niko tayari/siko tayari kutekeleza maagizo na kufuata sheria za shule

Sahihi ya Mwanafunzi ...................................

Tarehe ...................................

Mimi ........................................................................ (Mzazi/Mlezi) nimesoma na kuyaelewa mahitaji na sheria za shule kama zilivyoandikwa.

- Niko tayari/siko tayari kumruhusu mwanangu ................................................ kujiunga na shule aliyochaguliwa.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi .................................................... Tarehe ..................................

- Futa isiyohusika.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer in respect of all Form I and V entrants.

Student's full Name ..........................................................................................................

Age ................................................................. sex ....................................................

Blood found (red and white) ............................................................................................

Stool examinations ...........................................................................................................

Urinalysis ..........................................................................................................................

Syphilis and other .............................................................................................................

General Diseases test .......................................................................................................

T. B Test ...........................................................................................................................

Eye Test ............................................................................................................................

Ears Test ...........................................................................................................................

Chets ................................................................................................................................

Spleen ..............................................................................................................................

Abdomen ..........................................................................................................................

Urine for planet .................................................................................................................

Additional information (if any eg. Physical defects impartment (s) (eg. Arm leg etc) infections chronic or families disease etc.

.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/unfit to pursue further Execution on as stated above.

**Signature** ......................................................................................

**Designation** ...................................................................................

**Station** ..........................................................................................

**Date** .............................................................................................